WIZARA YA ELIMU,
SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MoEST Weekly

14 Januari, 2026



# ELIMU KIDIJITALI, HITAJI SIYO CHAGUO -PROF. NOMBO

# ELIMU KIDIJITALI, HITAJI SIYO CHAGUO -PROF. NOMBO

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amesema mabadiliko ya kidijitali si chaguo tena bali ni hitaji la lazima, kama inavyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (DIRA 2050).

**Prof. Nombo** ameeleza hayo Januari 14, jijini Dodoma akifungua Warsha ya kujenga uelewa wa pamoja juu ya Mkakati wa Kitaifa na matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika Elimu na Miongozo yake, akisisistiza kuwa Mkakati huo utaongoza mageuzi ya kidijitali katika ngazi zote za elimu.

"Teknolojia peke yake haiwezi kuleta mabadiliko ya kweli katika elimu bila walimu wenye ujuzi na utayari wa kutumia teknolojia za kufundishia na kujifunzia. Kwa hiyo, vyuo vya ualimu, vyuo vikuu na taasisi zote za mafunzo zinapaswa kujumuisha kwa makusudi ufundishaji wa kidijitali" amesema Prof. Nombo.

Amehimiza taasisi zote za elimu kushirikiana kwa karibu na Wizara ili kuhakikisha mshikamano wa kisera, ulinganifu na muingiliano wa mifumo na uzingatiaji thabiti wa sera na miongozo ya kitaifa.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, **Prof. Daniel Mushi** amesema mkakati wa kitaifa wa matumizi ya teknolojia za kidijitali katika elimu umezingatia ubora wa elimu, usawa wa fursa, ubunifu na matumizi yanayolenga teknolojia za kidijitali nchini.

Miongozo hiyo ni pamoja na Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika Elimu 2024/25 - 2029/30, Mwongozo wa Kitaifa wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika shule na vyuo vya ualimu na Mwongozo wa Kitaifa wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika vyuo vya ufundi na Mafunzo ya Ufundi stadi.

Mwingine ni Mwongozo wa Kiaifa wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika Vyuo Vikuu na Mwongozo wa Kitaifa wa Matumizi ya Akili Unde katika Elimu. Amehimiza ushirikiano na wadau ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kwa upande wake, Mkuu wa chuo cha Butimba, **Nicholaus Magige**, ameishukuru serikali kwa kuwajengea uwezo wakufunzi wa vyuo vya ualimu kuhusu matumizi ya teknolojia ikiwemo akili Unde, ambayo huwawezesha katika ufundishaji.

Naibu Mkuu wa Chuo cha Ufundi Arusha anayeshughulikia masuala ya taaluma, utafiti na ushauri **Dkt. Yusuph Mhando** amesema kuwa chuo hicho, tayari kimechukua hatua katika matumizi ta teknolojia ikiwa ni pamoja na kufundisha walimu wa TVET kwa njia ya mtandao.



*Prof. Carolyne Nombo*
*Katibu Mkuu*



*Prof. Daniel Mushi*
*Naibu Katibu Mkuu*



*Dkt. Alcardo Alex*
*Mratibu wa Elimu Kidijitali*

